**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**

**KISWAHILI 102/3**

**FASIHI**

**SWALI LA KWANZA**

i. Jitu linakula chakula chote katika hoteli ya mzee Mago na kuonyesha kutojali wengine.
ii. Jitu linanyakua ardhi ya maskini wa Madongoporomoka baada ya uvumi uliokuwa ukienezwa.
iii. Mzee Mambo hakuwa na kazi maalumu na waziri kivuli wa wizara zote aliyekuwa akilipwa mshahara.
iv. Kuna ubadhirifu wa mali umma kwani mambo anasherehekea mtoto wake kuingia nasari skuli na mwingine kutoa vijino viwili kwenye ufizi.
v. Viongozi wanapendelea mambo ya kigeni. Sasa na Mbura pamoja na viongozi wengine wanakula wali wa Basmati badala ya wali wa Mbeya.
vi. Mzee Mambo anafanya biashara na serikali kwani yeye ni mmiliki wa duka kubwa la dawa ambalo mtaji wake ni bohari kuu ya serikali.
vii. Jitu linasimamia kubomolewa kwa vibanda vya maskini wa madongoporomoka.
viii. Mzee Mambo na viongozi wengine wanapata huduma zote za msingi bure. Huduma hizo ni umeme,maji,matibabu na huduma nyingine.
ix. Wanasheria wanahongwa na viongozi ili kutotetea maskini kuhusu unyakuzi wa ardhi.
x. Sasa na Mbura wanazembea kazini kwani hawafuati mipango na mipangilio ya wizara zao.

( Hoja 10 x2)

**SWALI LA PILI**

2. (a) Haya ni maneno ya **mwandish**i akimrejelea **Mtemi Nasaba Bora** aliyetawazwa kuwa kiongozi wa **sokomoko** na kuanza uongozi mbaya.

(4x1)

(b) Muuaji – Alimuua Chichiri Hamadi.

Mwenye uzinifu- Alimfanya Lowela kuwa na mimba .

Mwenye hasira/mkali- Alifuta wafanyi kazi wake.

Fisadi –Alitoa hongo ili Madhubuti apate kazi ya jeshi.

Katili-Alimpiga Amani kikatili na kumtupa kando ya mto Kiberenge.

Wivu-Alitaka kuzungumza kama ndugu yake majisifu mwenye majuto.

(ZOZOTE 4X1)

(c) i. Mtemi Nasaba Bora aliwafuta wafanyikazi mara nyingi.

ii. Alimpagaza Amani mtoto Uhuru

iii. Alimpiga Amani na kumuacha kando ya mto Kiberenge

iv. Alilazimisha watu kama Bi. Kizee kuhudhuria siku ya wazalendo.

v. Alimpa mkewe Zuhura talaka.

vi. Alikataa kumpeleka DJ hospitali alipong'atwa na mbwa.

vii. alimlazimisha Amani kuchimba kaburi lake.

viii. Alizungumza kimombo wakati wa sherehe ya siku ya wazalendo.

ix. Alimpatia Lowela mimba.

xi. Aliwanyanganya wazazi wa Imani na Chichiri Hamadi shamba lao.

xii. Alikataa kumbeba mama mjamzito aliyekuwa njiani.

xiii. Alificha faili na kubadilisha hati akiwa wizara ya ardhi.

xiv. Aliudhika alipokosa picha yake katika gazeti ya Tomoko Leo.

xv. Alimwacha msichana kiwate aliyekuwa amezungumza naye garini.

xvi. Alitoa hongo ili Madhubuti apate kazi jeshini.

xvii. Aliwaweka Matuko Weye, Amani na Imani gerezani.

xviii. Alimzingizia Yusufu kuwa muuaji na kumfanya afungwe.

xix. Aliamrisha askari kumpiga mamake Imani na kuchoma nyumba yake.

(zozote 12 x 1)

**SWALI LA TATU**

i. Amani aliibiwa mswada wake wa Kidagaa Kimemwozea na kukosa matumaini lakini mwishowe alipata kujua aliyeiba ni mwalimu Majisifu.

ii. Shamba la Chichiri Hamadi aliyekuwa babu yake Amani, lilinyakuliwa na Mtemi Nasaba Bora lakinin mwishowe alilipata.

iii. Mtemi Nasaba Bora alimdharau Amani akiwa mfanyikazi wake lakini baadaye anamsifu na kumuomba msamaha kwa maovu aliyomtendea.

iv. Amani alikatiza masomo yake chuoni baada ya uchochezi wa wanafunzi wenzake mwishowe anarejelea chuo kikuu na kumaliza masomo yake.

v. Amani alifanya kazi ya kijungujiko akiwa mfanyakazi wa Mtemi mwishowe anapata ardhi na kuwa tajiri.

vi. Amani alipagazwa ulezi wa kitoto uhuru lakini inabainika kuwa mtoto ni wa Mtemi Nasaba Bora.

vii. Amani alipigwa na Mtemi Nasaba Bora na kuachwa kando ya mto Kiberenge hata hivyo anaokolewa na kupelekwa hospitali na baadaye kwa mwalimu Majisifu.

viii. Amani aliwekwa gerezani kwa tuhuma ya kuua kitoto Uhuru lakini anaachiliwa baada ya barua kutoka kwa Lowela.

ix. DJ anang'atwa na mbwa Jimmy na kupelekwa kupokea matibabu ambapo anapona na hata kushirikiana na Amani.

x. DJ hakuwa na makao kwani alikuwa ametoroka jela mwishowe anagawiwa ardhi na Amani.

(zozote 10 x 2)

**SWALI LA NNE**

a. Haya ni maneno ya Boza akimwambia Kombe wakiwa katika karakana iliyo kwenye soko la chapakazi na ni baada ya Sudi kukataa kula keki. (4 x 1)

b. Ngurumo – Alisema kura yake ni ya majoka.
Kenga-Alishughulikia kinyago cha Majoka. Ni mshauri wake.

Mama pima (Asiya) - Aliruhusiwa na Majoka kuuza pombe na alimsifu.

(3x2)

C

i. Tunu alipopinga Majoka alipangiwa njama akavunjwa mguu.

ii. Tunu alipoenda Mangweni aliingiliwa na Walevi kama Ngurumo na kuambiwa aende akaolewe.

iii. Siti na Bi.Hashima wanasema makaratasi yametandazwa ya kuwataka waondoke baada ya mwanawe Tunu kupinga Majoka.

iv. Sudi alipokataa kuchonga vinyago alipoteza kazi yake baada ya soko la chapakazi kufungwa.

v. Ashua alipokataa kazi ya ualimu katika Majoka and Majoka Academy na kuanza kazi ya kuuza madafu na chai alimtafuta Majoka kwa sababu ya umaskini.

vi. Ashua alipomkataa Majoka alitiwa gerezani baada ya kupigana na Husda.

vii. Ngurumo aliuawa baada ya kushindwa kutekeleza kazi aliyopewa wenzake ya kumuua Tunu.

viii. Jabali alipopinga majoka aliuawa na chama chake cha Mwenge kikamalizwa.

ix. Waandamanaji katika kiwanda cha Majoka and Majoka Company kama vijana watano walipigwa risasi.

x. Runinga ya Wazalendo ilipoonyesha maandamano ilifungwa ikabaki sauti ya wananchi.

(10x1)

**SWALI LA TANO**

a. Haya ni maneno ya **<u>Kenga</u>** anamwelezea **<u>Majoka</u>** wakiwa **<u>hoteli ya Majoka and Majoka Resort</u>** anapojiburudisha na mkewe Husda ni wakati Kenga alikuja kumwelezea Majoka kuwa **<u>mipango ya kumwangamiza Tunu</u>** haikutekelezwa vyema.

b. Tamko hili linamaanisha kuwa **<u>hawakumuua</u>** Tunu badala yake walivunja mguu wa kawaida. Tamathali iliyotumika ni **<u>Jazanda.</u>** ( 2x2)

c.

i. Jasiri- Aliandamana na Sudi hadi ofisi ya Majoka.
ii. Mwenye Busara- Alimweleza Majoka kwamba wao ndio waliopigania haki ya baada kifo cha babake.
iii. Mwenye msimamo thabiti- Alikataa mpango wa kuozwa kwa Ngao Junior.
iv. Mzalendo- Alipingana na Majoka dhidi ya kufunga soko la wanasagamoyo.
v. Mwenye utu/huruma- Alipeleka watoto wa Sudi kwa Bi.Hashima.
vi. Mtetezi wa haki- Anaitisha mkutano wa kufungua soko.

Zozote(6x1)

d.

i. Anaonyesha mchango wa vijana katika ukombozi.
ii. Kupitia yeye tunaona maovu ya viongozi kama Majoka.
iii. Anaonyesha nafasi ya mwanamke katika jamii.
iv. Anaonyesha shida zinazowakabili wanasagamoyo chini ya Majoka.

(zozote 3x2)

**SWALI LA SITA**

a. Huru/vue/masivina- halizingatii urari wa vina, mizani, mishororo na vipande.

( alama 1 x 2)

b. Malalamishi- kuhusu kuzaliwa watoto wakatili, wasiojijua na haramu

Kupoteza/ ukosefu wa utu

Usaliti

Uzinifu ( alama 4 x 1)

c. Vijana walio na nguvu waliozaliwa Afrika ni wasaliti wasioweka siri. Wanarudisha nyuma maendeleo na kusaliti wanaofanya kazi kwa bidii. ( alama 4 x 1)

d. Jazanda – Afrika ni mama

Uradidi/takriri- kwa nini…kwa nini

Msemo- pigwa mshangao

Mdokezo- kwa nini… (alama 3 x 2)

e. Kizazi kisichojiweza au kulemaa ( 1 x1)

f. Fanyia ukatili (1 x 1)

## SWALI LA SABA

i. Kuonyesha mataifa yapaswa kujitegemea.

ii. Tarbia – lina mishororo minne kila ubeti

Ukara – vina vya upande mmoja vinafana (vina vya mwisho) ilhali vya upande wa kati vinabadilika .

(2 x 1)

iii. Tusiombe wataalamu wa nje

Tufuate uongozi

Tushiriki kila kazi

Tujitolee kama shujaa atakinakavyo (3 x 1)

iv. Inkisari- (1 x 2)

i. Wongozi
ii. Alotimiza
iii. Alomkini
iv. Itakiwavyo
v. Ghaibu
vi. Wanachi (zozote 5 x 1)

v. Nchi ni ile ambayo imejikita ardhini si ile inayoomba ng'ambo na kwa majirani. Wananchi tuambianeni huo si utaratibu. Maganja ya mpewaji hukaa chini kila wakati. (4 x 1)

vi. Ghaibu- Ng'ambo

Tukamshabihi- Tukafanana (2 x 1)

## SWALI LA NANE

a. Miviga ni sherehe za kitamaduni ambazo hufanywa na jamii yoyote katika kipindi maalumu cha mwaka. (1 x2)

b.

i. Huandamana na matendo
ii. Huongozwa na watu mahususi
iii. Huandamana na utoaji wa mawaidha.
iv. Maleba maalumu huvaliwa na wanaohusika ili kuwatofautisha na hadhira.
v. Miviga hufanyiwa mahali sherehe hiyo inapofanyiwa
vi. Huambatana na utamaduni wa jamii husika.
vii. Huhusisha maombi, nyimbo, maghani, dua, kutukuza na kushukuru.
viii. Mara nyingi sadaka za vitu, mazao au wanyama hutolewa.
ix. Huweka nadhiri au ahadi ya kutenda mambo Fulani.
x. Hufanywa kwa lugha Fulani inayoandamana na sherehe.

(8 x 1)

c.

i. Huhatarisha afya na maisha ya watu. Mfano: kutiwa unyagoni.
ii. Huvunja haki za watu na kuzorotesha maendeleo
iii. Hujaza watu hofu.
iv. Miviga mingine huhusisha ushirikina.
v. Hugharimu pesa nyingi. (4 x 1)

d.

i. Huelimisha
ii. Ni kitambulisho cha jamii
iii. Huhifadhi utamaduni.
iv. Hukuza uzalendo
v. Hukuza umoja.
vi. Hutuliza waombolezaji
vii. Hutoa maadili.
viii. Husaidia jamii kukabiliana na hali ngumu.
ix. Huonyesha kuvuka daraja moja la maisha hadi lingine.
x. Huhifadhi historia.
xi. Hukuza lugha.
xii. Hukuza stadi na vipawa.

( 6 x 1)